

JUMUIYA KUUNGANA NA KUENDESHA GARI KWA KIASI

TOA ATHARI CHANYA KWA JAMII YAKO

Tengeneza Mpango timamu wa dereva aliye na Leseni: hakuna gharama na inaokoa maisha

Ulevi ni Kiasi cha Pombe kwenye damu (BAC).08 asilimia au zaidi. **BAC** ya asilimia.08 au zaidi ni ushahidi wa ulevi, na **BAC** ya asilimia.18 au zaidi ni ushahidi wa uendeshaji kasi wakati umelewa. Mtu anaweza kuwa mlevi kwa kunywa pombe.

Ulevi ni matokeo ya madawa yoyote mwilini mwako ambayo yanakufanya ushindwe kutumia maamuzi sahihi ya kuendesha gari. Madawa hayo yanaweza kuwa pombe, madawa ya famasia au yasiyo ya famasia. Kiasi cha Pombe Damuni (**BAC**) cha zaidi ya asilimia .05 ni ushahidi wa kisheria kuwa umelewa.

Utimamu ni kutokuwa chini ya kilevi chochote cha madawa au pombe. Dereva aliye timamu ni mtu ambaye hana pombe au madawa yoyote na anayo leseni na uwezo wa kuendesha gari.

Weka Mipango

Dereva Timamu aliye na Leseni:

- Kila wakati endesha gari na dereva timamu aliye na leseni, dereva ambaye hakuwa akinywa pombe au asiye na kilevi cha madawa.
- Kama sherehe zinahusisha pombe weka mipango kabla ya kwenda ya nani atakayekuwa dereva timamu aliye na leseni ya uendeshaji.
- Kuwa rafiki mzuri na uliza kama unafikiri kuna mtu mlevi au amelewa. Saidia kutafuta dereva mwenye leseni aliye timamu au ita taxi kwa usafiri salama. Usiwaruhusu kuendesha.
- Watoto ni lazima wakati wote waendeshwe na dereva mwenyealiye timamu. Weka mipango ya kuwalinda watoto kutokana na madereva walevi au waliolewa
- Madereva walevi au waliolewa wakiwa na watoto chini ya umri wa miaka 16 ndani ya gari wanaweza kushitakiwa chini ya sheria ya Leandra, jinai.


TAMBUA GHARAMA ZA KUENDESHA UKIWA MLEVI/UMELEWA (DWI)

ULEVI WA POMBE AU KULEWA KWA MADAWA

Kuendesha Wakati Umelewa/Mlevi (DWI) inaumiza watu, familia na jamii. Ajali zinatokea na watu wasio na hatia wanaweza kuumizwa au kufa. Sheria ya kulinda watu kutokana na madereva walevi/waliolewa ni madhubuti na inagharimu sana. Watu walioshitakiwa na DWI wanaweza kwenda jela, kukatazwa kuendesha gari, kupoteza kazi zao na wanaweza kupata athari za uhamiaji wao.

KUKAMATWA NA KUFUNGWA / KUSHITAKIWA KWA UHALIFU/ JELA/PIGA SIMU

KUCHOTA GARI/ADA YA KUHIFADHI.....	\$300,00
JELA NA DHAMANA.....	\$500,00
MWANASHERIA WA JINAI.....	\$1000,00-\$5000,00
MWANASHERIA WA UHAMIAJI.....	\$??????
FIDIA/ NYONGEZA.....	\$250,00-\$2000,00
KIWASHO ZUIA.....	\$150,00
TATHMINI YA POMBE.....	\$150,00
ATHARI ZA JOPO LA WAHANGA.....	\$50,00
USIMAMIZI WA JARIBIO.....	\$250,00
DDP.....	\$175,00
DMV ADHABU YA KIRAI.....	\$200,00
LESENI ILIYO NA MASHARTI.....	\$100,00
UPIMAJI (KILA BAADA YA MIAKA 3).....	\$250,00
BIMA YA MAGARI.....	?????
JUMLA YA BEI LEBO.....	\$10 000,00 +



UWEZEKANO WA GHARAMA NYINGINE:

UPOTEVU WA MAISHA YAKO AU YA WENGINE

UPOTEVU WA UHURU

ATHARI ZA UHAMIAJI

- Vikwazo vya kupata Kadi ya Kudumu na Uraia
- Kuwekwa nafasi ya Kesi za Kuondolewa
- Kufukuzwa na serikali ya Marekani